HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti,

**BARAZA LA MADIWANI**

# TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) MWAKA WA FEDHA 2024/2025 TAREHE 06/11/2024

## UTANGULIZI

**Mhe. Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii imegawanyika katika Maeneo yafuatayo: -

1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA KWANZA
2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA KWANZA

**2.1 MAPATO YA NDANI**

2.1.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Mapato ya Ndani zilizovuka mwaka 2023/2024

2.1.2 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Mapato ya Ndani Bajeti ya 2024/2025

**2.2 SERIKALI KUU**

2.2.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Serikali Kuu zilizovuka mwaka 2023/2024

2.2.2 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Serikali Kuu kwa bajeti ya 2024/2025



CamScanner

3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA
4. HITIMISHO

## 1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA KWANZA

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri yetu imekusudia kukusanya kiasi cha 14,953,399,100.00 katika bajeti ya mapato ya ndani, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Septemba mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 3,785,442,355.00 sawa na asilimia 25 ya lengo la mwaka na sawa na asilimia 100 ya lengo la Robo.

## 2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA KWANZA

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Mwaka 2024/2025, Halmashauri imeidhinishiwa kutumia shilingi 17,024,038,046.20, ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024 Halmashauri imepeleka kiasi cha shilingi 6,152,316,020.88 sawa na 36.1% kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao;

### 2.1 MAPATO YA NDANI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa robo ya kwanza, jumla ya shilingi **2,420,463,106.82** zilielekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zetu ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 1,033,835,774.15 ni fedha za mapato ya ndani zilizotolewa mwishoni mwa mwaka na fedha zilizovuka mwaka, na shilingi 1,386,627,332.67 ni fedha za mapato ya ndani kwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025.

#### 2.1.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Mapato ya ndani zilizovuka mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti;** katika kipindi hiki fedha zilizotolewa mwishoni mwa mwaka na zilizovuka mwaka ni shilingi 1,033,835,774.15 na zimeelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ifuatao;

i. Shilingi 317,335,774.15 kwa ajili ya Fidia ya Ardhi.

ii. Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Hospitali ya Wilaya

iii. Shilingi 40,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa jengo la mama na mtoto Zahanati ya Nyakato

iv. Shilingi 40,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa uzio Shule ya Misingi Kitangiri

v. Shilingi 35,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa Hostel ya watoto wenye mahitaji maalum Buswelu S/M

vi. Shilingi 30,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Nyasaka

vii. Shilingi 30,000,000.00 kwa ajili ya Umaliziaji wa Maabara Zahanati ya Kahama

viii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 2 Kiloleli S/M

ix. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 2 Umoja S/M

x. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 2 Bugogwa S/M

xi. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 2 Lumala Sekondari

xii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa Zahanati Bwiru

xiii. Shilingi 24,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 3 Shule ya Sekondari Mnarani

xiv. Shilingi 22,800,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi Ofisi ya Kata ya Mecco

xv. Shilingi 16,000,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya mitaro Eneo la makaburi na kufanya jumla ya shilingi 21,000,000.00 zilizotolewa kwa shughuli hii

xvi. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa choo, incinirator na Placenta pit katika Zahanati ya Kawekamo

xvii. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa Ofisi ya Mtaa wa Kilimahewa "A

CamScanner

i. Shilingi 400,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Ilemela
ii. Shilingi 262,369,781.70 kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu
iii. Shilingi 140,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Wodi ya Wazazi Zahanati ya Nyakato
iv. Shilingi 136,167,966.85 kwa ajili ya fidia ya Ardhi
v. Shilingi 118,000,000.00 kwa ajili ya malipo ya greda awamu ya kwanza
vi. Shilingi 37,500,000.00 kwa ajili ya malipo ya kijiko(mtambo) awamu ya kwanza
vii. Shilingi 70,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha Afya Kayenze
viii. Shilingi 60,228,500.00 kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la Utawala
ix. Shilingi 39,600,000.00 kwa ajili ya usafishaji mji na udhibiti taka
x. Shilingi 37,505,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Hosteli ya wanafunzi wenye mahitaji maalum S/M Buswelu
xi. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa chumba cha X-ray kituo cha Afya Buzuruga
xii. Shilingi 24,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule ya Sekondari Angelina Mabula
xiii. Shilingi 10,445,832.00 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 150 kwa ajili ya Shule za Misingi
xiv. Shilingi 7,964,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa choo kipya na ukarabati wa choo cha zamani katika uwanja wa Furahisha
xv. Shilingi 6,490,000.00 kwa ajili ya gharama za Maonyesho ya Nane Nane
xvi. Shilingi 5,468,252.12 uendeshaji na ukatabati wa miundombinu ya stendi (O & M)
xvii. Shilingi 3,900,000.00 kwa ajili ya ununuzi na upandaji Miti 1500

CamScanner

xviii. Shilingi 1,988,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa vyoo Mialo ya Igombe na Kabangaja

## 2.2 SERIKALI KUU

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa robo ya kwanza, jumla ya shilingi **3,731,852,914.06** zimepokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zetu ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 2,035,060,418 ni fedha za miradi iliyopokelewa mwishoni mwa mwaka 2023/2024, na shilingi 1,696,792,496.06 ni fedha za miradi ya Ruzuku kutoka Serikali kuu kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.2.1 UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA FEDHA ZA SERIKALI KUU ZILIZOVUKA MWAKA 2023/2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti**; katika kipindi hiki fedha zilizopokelewa mwishoni mwa mwaka na zilizovuka mwaka ni shilingi 2,035,060,418 na zimeelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ifuatao;

i. Shilingi 584,280,209.00 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Masemele

ii. Shilingi 584,280,209.00 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Kilabela

iii. Shilingi 351,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi mpya ya mkondo mmoja Masemele

iv. Shilingi 260,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Mabweni 2 katika shule ya Wavulana Bwiru

v. Shilingi 155,500,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 ya awali ya mfano, matundu 12 ya vyoo, vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Kayenze Ndogo

vi. Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya mwalimu (2 in 1) katika shule ya Sekondari Kisenga

CamScanner

### 2.2.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA BAJETI YA 2024/2025

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa robo ya kwanza, jumla ya shilingi 1,696,792,496.06 fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu zilipokelewa na kuelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa mchanganuo ufuatao;

i. Shilingi 1,162,712,951.00 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya lami Buswelu-Nyamadoke-Nyamhongolo 9.4 km na Buswelu-Busenga-Coca cola 3.3 km
ii. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Afya Zahanati ya Bezi mtaa wa Tefu
iii. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa OPD mtaa wa Bezi
iv. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu ya familia mbili mtaa wa Iseni Kayenze sekondari
v. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa OPD Zahanati ya Luhanga Kata ya Kiseke
vi. Shilingi 87,158,076.29 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wavulana 80 shule ya sekondari Kayenze kuanzia msingi hadi upauaji mtaa wa Kayenze
vii. Shilingi 77,278,611.61 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wavulana 80 shule ya sekondari Kayenze kwa hatua ya umaliziaji mtaa wa Madukani

## 3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 02/07/2024, Mheshimiwa Dkt. Daniel Damas Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo alitembelea Halmashauri yetu ambapo alipata fursa ya kukagua Uwanja wa CCM Kirumba ambao ni uwanja wa pili kwa ukubwa Tanzania wenye uwezo wa kibeba watu 35,000. Pia, alifika Kata ya Buswelu kwenye eneo linalotarajiwa kujengwa Kituo

cha ufundishaji na kujifunzia michezo kwa ubora (sports academy and centre of excellence).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 06/07/2024, Mheshimiwa Angelina Lubala Mabula alipokea jumla ya mitungi 500 kutoka katika Kampuni ya ORYX na aliigawa kwa makundi mbalimbali ya wananchi wa Wilaya ya Ilemela.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo Tarehe 12/07/2024 Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Said Mtanda alikabidhiwa vyumba 59 vya madarasa na matundu 72 ya vyoo katika shule za sekondari kwenye Halmashauri yetu. Mradi huu umegharimu shilingi 1,417,100,000.00 fedha za Programu ya BOOST kutoka Serikali Kuu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo Tarehe 15/07/2024 Matokeo ya kidato cha sita yalitangazwa ambapo ufaulu katika shule za Halmashauri yetu umeongezeka kutoka asilimia 99.9 kwa mwaka 2023 hadi asilimia 100 kwa mwaka 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 02/08/2024 Baraza la Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri yetu walimchagua Mhe. Manusura Sadick Lusigalile, Diwani wa Kata ya Buzuruga kuwa Naibu Meya wa Manispaa ya Ilemela kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ushindi kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 08/08/2024 Halmashauri yetu ilipokea tuzo katika Maonyesho ya Nane Nane kwa kushika nafasi ya pili katika kundi la Taasisi za Serikali za Mitaa zilizoshiriki maonesho ya Kilimo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 21/08/2024 hadi tarehe 27/08/2024 Halmashauri yetu ilishiriki katika zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa kata zote 19.

CamScanner

cha ufundishaji na kujifunzia michezo kwa ubora (sports academy and centre of excellence).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 06/07/2024, Mheshimiwa Angelina Lubala Mabula alipokea jumla ya mitungi 500 kutoka katika Kampuni ya ORYX na aliigawa kwa makundi mbalimbali ya wananchi wa Wilaya ya Ilemela.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo Tarehe 12/07/2024 Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Said Mtanda alikabidhiwa vyumba 59 vya madarasa na matundu 72 ya vyoo katika shule za sekondari kwenye Halmashauri yetu. Mradi huu umegharimu shilingi 1,417,100,000.00 fedha za Programu ya BOOST kutoka Serikali Kuu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo Tarehe 15/07/2024 Matokeo ya kidato cha sita yalitangazwa ambapo ufaulu katika shule za Halmashauri yetu umeongezeka kutoka asilimia 99.9 kwa mwaka 2023 hadi asilimia 100 kwa mwaka 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 02/08/2024 Baraza la Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri yetu walimchagua Mhe. Manusura Sadick Lusigalile, Diwani wa Kata ya Buzuruga kuwa Naibu Meya wa Manispaa ya Ilemela kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ushindi kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 08/08/2024 Halmashauri yetu ilipokea tuzo katika Maonyesho ya Nane Nane kwa kushika nafasi ya pili katika kundi la Taasisi za Serikali za Mitaa zilizoshiriki maonesho ya Kilimo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 21/08/2024 hadi tarehe 27/08/2024 Halmashauri yetu ilishiriki katika zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa kata zote 19.

CamScanner

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 27/08/2024 Halmashauri yetu ilipokea gari aina ya hilux double cabin DFPB 0402 kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za mradi wa TACTIC kutoka Serikali Kuu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 29/08/2024 Halmashauri yetu ilisaini mkataba wa ununuzi wa matipa mawili kwa ajili ya kuwezesha shughuli mbalimbali za Halmashauri. Mkataba huu umesainiwa kati ya Halmashauri yetu na Kampuni ya PUMALogistic Solution LTD ya Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 30/08/2024 Mtahiki Meya wa Manispaa yetu aliongoza mkutano maalum wa baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa ya ufungaji wa hesabu za mwisho za mwaka wa fedha 2023/2024.

## 4. HITIMISHO

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri yetu, viievile tunapenda kumshukuru Mhe. Mbunge Angelina S. Mabula kwa kuendelea kuchochea na kuhamasisha utekelezaji wa Miradi katika Halmashauri yetu, pia tunamshukuru Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Wananchi wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Miradi ya Manispaa ya Ilemela.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Naomba kuwasilisha.

Ummy M. Wayayu

**MKURUGENZI WA MANISPAA**

**ILEMELA**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
S.L.P. 735
MWANZA.

CamScanner